SIGNAL Publishers
Igniting thinking

# DARASA LA NANE

**SIGNAL 003**

# SIGNAL EXAMS 2020
# JARIBIO LA TATU

## KISWAHILI
## SEHEMU YA KWANZA:
## LUGHA

**Muda: Saa 1 dakika 40**

### SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibu. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu andika katika kijitabu hiki.
3. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala sio katika kijitabu hiki cha maswali.

### JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU

4. Tumia penseli ya kawaida.
5. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu:

   **NAMBA YAKO YA MTIHANI**
   **JINA LAKO**
   **JINA LA SHULE YAKO**

6. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule, na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu.

9. Kwa kila swali 1 – 50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C na D. Ni jibu **MOJA** tu kati ya hayo manne ambayo ni sahihi. Chagua jibu hilo.

10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.
**Mfano**
**Katika kijitabu cha maswali:**

**11.** Watu waliofikwa na msiba wa kifo huamkiwaje?
A. Poleni.
B. Mwaambaje?
C. Makiwa.
D. La utu?
Jibu sahihi ni C. **(makiwa)**

Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba 11, kisanduku chenye herufi C ndicho kilichochorwa kistari.

1 [A] [B] [C] [D]   11 [A] [B] [C] [D]   21 [A] [B] [C] [D]   31 [A] [B] [C] [D]   41 [A] [B] [C] [D]

11. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
12. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku kimoja tu kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**Kitabu hiki cha maswali kina kurasa 7 zilizopigwa chapa**

SIGNAL

© *Signal Publishers Limited 2020*
*Website: www. signalpublishers.com. Email. info@signalpublishers.com*

SignalPublishers @SignalPublishers

**Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne. Jaza kila pengo kwa kuchagua jawabu lifaalo zaidi.**

Maria___1___ kwa huzuni kuu. Kasri ___2___ kuwa jehanamu kwake. Mjomba wake alikuwa amemchukua ili kumpa ___3___ wa kimasomo baada ya wavyele wake kufariki. Kila uchao ___4___ na vitimbi vya kila aina.___5___hayo yote, jambo moja lilimtia Maria ari ya kushikilia mpaka mwisho. Alijua kuwa ___6___ hizi ni za muda tu kwani ___7___. Alikuwa karibu kuhitimisha masomo yake. Alijua kwamba elimu ___8___ngao yake ya pekee ya kujihami na dhuluma za aina hii.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | A. alikula mwande | B. alijishika tama | C. alijipiga jeki | D. alitia hamnazo |
| **2.** | A. humo mligeuka | B. hiyo iligeuka | C. hilo paligeuka | D. hilo liligeuka |
| **3.** | A. ufadhili | B. udhalimu | C. dhamana | D. uthamini |
| **4.** | A. alikabidhiwa | B. alijaliwa | C. alikabiliwa | D. alifarakana |
| **5.** | A. Licha ya | B. Dhidi ya | C. Bighairi | D. Baina ya |
| **6.** | A. shinda | B. dhiki | C. matatizo | D. utesi |
| **7.** | A. mbwa hafi maji aonapo ufuko | B. papo kwa papo kamba hukata jiwe | C. pavumapo paliliesi kazi kudamirika | D. hakuna marefu yasiyokuwa na ncha |
| **8.** | A. ndiyo iliokuwa | B. ndio iliyokuwa | C. ndiyo iliyokuwa | D. ndilo lililokuwa |

Vijana wengi wameonekana ___9___ katika sanaa ya uimbaji na uigizaji katika siku za hivi karibuni. Wao hujiunga na ___10___ mbalimbali ___11___ tu wajizumbulie riziki. Hii ni hatua mwafaka ya kupunguza uhaba wa ajira. Isitoshe, ni mojawapo ya njia ___12___ utamaduni wetu. Hata hivyo, tatizo ___13___ hapa ni kuwa baadhi ya vijana hawa ___14___ fani hii kwa lengo la kuchuma tu. Wao huwa ___15___ kufanya lolote linalowaletea chumo hata kama linakiuka maadili.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **9.** | A. kujitosa | B. kujitoma | C. kujiweka | D. kutoweka |
| **10.** | A. vikosi | B. vikoa | C. vigaro | D. vipeto |
| **11.** | A. ilhali | B. japo | C. lau | D. alimradi |
| **12.** | A. inayokuza | B. zinazokuza | C. inazokuza | D. zinaokuza |
| **13.** | A. lililoko | B. liliyopo | C. lililopo | D. lililomo |
| **14.** | A. wameingilia | B. wangeingilia | C. wakaingilia | D. wakiingilia |
| **15.** | A. hadhi | B. heri | C. bora | D. radhi |

***Kuanzia nambari 16 mpaka 30, chagua jawabu lifaalo zaidi.***

16. Chagua kiingizi kinachoashiria furaha.
A. Inshallah! B. Lahaula!
C. Shabash! D. Wallahi!

17. **Andika wingi wa sentensi ifuatayo.**
Uta uliotumiwa na jangili umepatikana.
A. Nyuta iliyotumiwa na jangili imepatikana.
B. Nyuta zilizotumiwa na jangili zimepatikana.
C. Nyuta zilizotumiwa na wajangili zimepatikana.
D. Nyuta zilizotumiwa na majangili zimepatikana.

18. Ni ipi sentensi changamano kati ya hizi?
A. Sote tuna haki ya kuenda shule.
B. Wanafunzi waliofanya bidii wametunzwa.
C. Nilimweleza ukweli lakini akanipuuza.
D. Tulikimbia sana ili tusinyeshewe.

19. Bainisha sentensi iliyoakifishwa ipasavyo.
A. Rununu, simu ya mkononi, imerahisisha mawasiliano.
B. Alinunua nyanya, mboga, vitunguu, na viazi.
C. Lo, umetoka mjini kwa miguu?
D. Wametueleza ukweli........hatuna haja ya ugomvi.

20. Kisigino ni kwa mguu kama ilivyo kiwiko kwa
A. kichwa B. shingo
C. wayo D. mkono

21. Chagua sentensi iliyotumia kiambishi <u>ka</u> kuonyesha kufuatana kwa matukio.
A. Uzi ulikatika akishona nguo.
B. Nenda ukalifue shati hilo.
C. Nguo ilipigwa pasi ikanyoka.
D. Juma ameingia darasani akasome.

22. **Tegua kitendawili kifuatacho.**
Nikiita baba huitika 'baba'.
A. Radi B. Mwangwi
C. Kioo D. Pango.

23. Ainisha maneno yaliyoangaziwa kwenye sentensi ifuatayo.
Watoto walitahadharishwa **dhidi** ya kuchezea **barabarani**.
A. Kivumnishi, kiwakilishi.
B. Kiunganishi, nomino.
C. Kihusishi, nomino.
D. Kihusishi, kielezi.

24. Neno lipi lina silabi tano?
A. Shtaki B. Amekileta
C. Walishirikiana D. Maktaba

25. Mtu ambaye huwabebea watu mizigo kwa malipo huitwaje?
A. Mpagazi B. Mzegazega
C. Dalali D. Sonara

26. Vitamkwa vinavyokadiria urefu wa mishororo katika shairi huitwaje?
A. Silabi B. Vina
C. Mizani D. Arudhi

27. **Geuza sentensi ifuatayo katika usemi wa taarifa.**
Kibe: Mwanangu, ukiishi kwa uadilifu utaheshimika maishani.
A. Kibe aliambiwa na mwanawe kuwa akiishi kwa uadilifu ataheshimika maishani.
B. Kibe alimwambia mwanawe kuwa iwapo ataishi kwa uadilifu ataheshimika maishani.
C. Kibe aliambiwa kuwa iwapo angeishi kwa uadilifu ataheshimika maishani.
D. Kibe alimwambia mwanawe kuwa iwapo angeishi kwa uadilifu angeheshimika maishani.

28. Sentensi ipi imetumia **<u>nomino ya dhahania</u>?**
A. Maji yale yametekwa mtoni.
B. Unyamavu wake hauonyeshi kutojua.
C. Kusoma kuna manufaa mengi.
D. Kitabu hicho kina michoro mizuri.

29. **<u>Chafua</u>** ni kwa **<u>uchafu</u>** kama ilivyo **<u>cheka</u>** kwa
A. ucheshi B. kucheka
C. chekesha D. chekwa

30. **'<u>Wa</u>' katika sentensi ifuatayo imetumikaje?**
Mkoba wa Kamene umepatikana.
A. Kuonyesha matumizi.
B. Kuonyesha uhusiano.
C. Kuonyesha umilikaji.
D. Kuonyesha kitendo.

**_Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 - 40._**

Mnamo siku za hivi karibuni, vimeshuhudiwa visa vingi vya utovu wa nidhamu katika shule zetu. **Si ibra** kusikia kuwa wanafunzi wamechoma shule au wametoroka na hata kuwadhulumu walimu wao. Katika kisa kimoja kilichoripotiwa, wanafunzi waligoma eti kwa kudai 'haki' kadhaa. Miongoni mwake walitaka kibali cha kuwa wakienda densi kila ijumaa na kutazama runinga kila siku kuanzia saa tatu usiku. Zaidi ya yote waruhusiwe kuvalia viatu watakavyo bila kudhibitiwa. Jambo hili lilishangaza sana. Utovu wa nidhamu shuleni huchangiwa na sababu anuwai.

Tangu kupigwa marufuku kwa adhabu ya kiboko, mambo yamekuwa mengine shuleni. Wanafunzi wamekuwa watundu na mradi wanajua hakuna kiboko, basi hawana cha kuhofia. Mihadarati pia imechangia pakubwa katika utovu wa nidhamu shuleni. Hizi sio zama ambazo mihadarati ilikuwa adimu sana. Sasa inapatikana kwa urahisi na kwa bei nafuu. Hivyo baadhi ya wanafunzi walio shuleni tayari wamebobea katika uraibu. Inakuwa vigumu kwa wanafunzi kama hawa kutii. Wengine hata hawaelewi lolote na hivyo wanakata tamaa na kutafuta faraja yao kwenye dawa hizi.

Utashangaa kuwa siku hizi mwanafunzi anayesifika sana shuleni sio yule bingwa wa masomo bali ni yule anayesumbua zaidi. Hili limewafanya wengi kukiuka maadili katika jitihada za kujizolea sifa. Wengine hata huingia kwenye maafa ya utovu wa nidhamu kwa sababu ya shinikizo la rika. Sio kwamba wenyewe huwa wamefikiria bali hufanya mambo kwa kufuata rubaa ya wenzao tu.

Teknolojia ni kiini kingine. Wapo wanafunzi wanaotoroka shuleni kwenda kushiriki vitendo visivyofaa. Wanafanya hivyo ili kufuatilia mambo wanayojifunza kupitia mitandaoni. Pia, wanafunzi wa siku hizi sio kama wale wa zamani waliokuwa wamejaa msukumo wa kufaulu katika maisha. Wapo waliokosa matumaini shuleni hivyo basi azima yao ni kuwavuta wengine upande wao.

Wanafunzi wengine huleta shuleni utovu wa nidhamu ambao huwa wameupata kutoka manzilini mwao. Wavyele wa siku hizi daima wamo mbioni kutafuta pesa hivyo basi utawapata chengoni kwa nadra sana. Ukiwauliza kuhusu wanao watakuelekeza ukamhoji kijakazi. Jambo hili linawafanya watoto kukosa adabu mapema. Baadhi ya wanafunzi wanalelewa katika mazingira yenye athari hasi kwao. Iwapo mtoto atalelewa kule kusikozingatiwa nidhamu, **<u>si ajabu akigeuka kuwa bendera na kufuata upepo</u>**. Ni vyema mtoto afunzwe kuwa si lazima atende kila atakalo.

Ulitima huwapelekea wengine kukosa nidhamu. Iwapo hawapati kiasi cha fulusi. cha fulusi wanachokitaka, wanaishia kuwa na mkono mrefu. Wengine huiba vitu vya wenzao kwa kushindwa kujipatia vyao binafsi. Vivyo hivyo, kuna wale watakaokosa kuadilika kwa sababu ni matajiri. Kiasi kikubwa cha masurufu wapatacho huwawezesha kugharamia hata starehe zisizofaa katika umri wao.

Kadhalika, kudorora kwa uhusiano kati ya walimu na wanafunzi ni chanzo kingine. Kwingineko, wanafunzi watakaidi amri kimakusudi ili wawaudhi walimu au walipize kisasi. Uhusiano huu ukichungwa labda mambo yanaweza kubadilika kuwa mazuri.

Baadhi ya nyimbo wanazosikiliza wanafunzi huhimiza mambo yaliyo kinyume na maadili. Mkengeuko huu unaleta madhara makubwa kwa wanafunzi. Isisahaulike kuwa wengi huwa katika umri wa kubaleghe. Wanafunzi katika umri huu huingilia matatizo kwa kutaka kujaribu hiki na kile.

31. Chagua jawabu lililo sahihi.
A. Awali hakukuwa na visa vyovyote vya utovu wa nidhamu.
B. Hali ya nidhamu inazidi kuimarika katika shule zetu.
C. Maadili ya wanafunzi yamezorota ikilinganishwa na awali.
D. Visa vya utovu wa nidhamu shuleni si vingi kama zamani.

32. Maneno **si ibra** jinsi yalivyotumika yana maana sawa na
A. si ajabu
B. si vigumu
C. inashangaza
D. ni ajabu

33. Wanafunzi wanaorejelewa katika aya ya kwanza
A. walipinga ukandamizaji wa walimu
B. walichoma shule na kuandamana
C. walitaka kanuni za shule zibadilishwe
D. walizuiwa kuvaa viatu na kushiriki starehe.

34. Si kweli kusema kuwa,
A. kuhofia matokeo ni njia mojawapo ya kudhibiti tabia
B. wanafunzi hawapewi adhabu shuleni sasa
C. ni rahisi kupata mihadarati kuliko awali
D. baadhi ya starehe huchangia kupotoka kwa wanafunzi.

35. Mambo yafuatayo huchangia matumizi ya mihadarati ila
A. kuwa na pesa nyingi za matumizi
B. mtu kupoteza matumaini maishani
C. kupewa maelekezo yafaayo maishani
D. kuiga nyendo za walio karibu nasi.

36. Wanafunzi wa zamani
A. hawakukabiliana na changamoto masomoni
B. walijawa na ari ya kufanikiwa maishiani
C. walitatizwa sana na shinikizo la rika
D. walishiriki maovu mengi sana shuleni mwao.

37. Msimamo wa mwandishi ni kuwa
A. tabia huathiriwa na kule alikolelewa na jinsi alivyokuzwa mtu
B. watoto wasipopewa pesa hawatakuwa na mienendo hasi.
C. kuiga jambo lolote huwa na madhara makubwa maishani
D. kudhibiti uhuru wa wanafunzi kumevuruga maadili shuleni.

38. ***'Si ajabu akigeuka kuwa bendera na kufuata upepo,'*** maana ya kifungu hiki ni kuwa
A. mtoto ataiga anayoyaona kwenye vyombo vya habari
B. mtoto atatenda atakalo bila kuulizwa na yeyote
C. mtoto ataenda huku na kule kama ifanyavyo bendera
D. mtoto atapotoka kimaadili kama wanajamii wengine.

39. Aya ya saba imeonyesha wazi kuwa
A. kuingiliana vyema kwa walimu na wanafunzi kutaboresha maadili
B. walimu hawataki kabisa kuwasikiliza wanafunzi shuleni
C. amri wanazotoa walimu ni muhali kufuatwa na wanafunzi
D. walimu wanaolipiza kisasi wamezua chuki kwa wanafunzi.

40. Umri wa kubaleghe una athari gani kulingana na kifungu?
A. Kusikiliza muziki ulio kinyume na maadili.
B. Kuleta mabadiliko yanayofanya mtu kuchanganyikiwa.
C. Kujaribu mambo ambayo huenda yakaleta madhara.
D. Kuvurugana na wazazi wasiotaka kuwa nyumbani.

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41 - 50.**

Tumaini alipojiunga na shule yetu, alifahamika mara moja kutokana na hali yake. Miguu yake yote miwili ilikuwa imelemaa, hali iliyomfanya kutumia kiti cha magurudumu. Japo walikuwepo wanafunzi wengine wenye ulemavu wa kiasi, hali yao haikuwa kitu ikilinganishwa na hii yake. Licha ya hayo, siku zote alionekana mwanafunzi mwenye bashasha aliyeingiliana vyema na wenzake na hata kuyachangamkia masomo yake vizuri. Ajabu ya ajabu ni kuwa sisi ndisi tulioonekana kumhurumia kwa hali yake ilhali yeye alionekana kana kwamba hata hakuwa na habari kuhusu udhaifu tuliouona.

Mwalimu mkuu alifanya mabadiliko katika baadhi ya miundomsingi ili kurahisisha maisha ya Tumaini na yeyote ambaye angejipata katika hali kama yake. Choo kimoja kilikarabatiwa na kufanywa cha kutapisha badala ya kuwa na lindi kama vinginevyo. Pia sakafu ilirekebishwa ili pawe na sehemu bora ya kupandishia vitimaguru mbali na vile vidato vya kawaida. Wanafunzi wengine nao walikuwa tayari kumpa Tumaini muwana popote alipohitaji japo yeye mwenyewe alionekana kujimudu kwa mengi. Hakika, Mola akikupa kilema hukupa na mwendo wake pia.

**Maulana alimtunuku Tumaini kichwa chepesi** kilichosheheni hazina ya maarifa. Kama angekosa nambari ya kwanza darasani basi ya pili isingemponyoka. Hili ndilo lililozidisha umaarufu wake miongoni mwa walimu. Tumaini alikuwa amedhihirisha wazi kwamba udhaifu wa viungo katu si kizingiti cha kuzuia mafanikio maadamu penye nia pana njia.

Naikumbuka siku moja nilipogombana na mwenzangu darasani. Huyu aliitwa Dama. Alikuwa amenicheka kwa uchochole wangu eti suruali yangu ilichanika karibu na goti. Nilipandwa na kiruu nikataka kumzaba vibao ili ajue kwamba sikuwa wa kuchezewa. Tumaini alizuka ghafla kivali kilipokuwa karibu kuzuka. "Mbona mnagombana marafiki zangu? Akasaili Tumaini. Nilimweleza nususi ya mambo naye akaangua kicheko. Nilimtazama kwa mshangao nikistaajabu iwapo naye pia aliicheka hali yangu.

"Sikilizeni," akaanza Tumaini. "Hapana tajiri wala maskini hapa. Kwanza hali yetu sote ni sawa. Je, kwani unamiliki nini unachoweza kuita chako? Mali ya wazazi si yako. Tunachohitaji ni kufanya bidii ili tuutawale ulimwengu wa kesho. Elimu inatupa nafasi ya kuuwekea **mustakabali** wetu msingi thabiti. Tukiitana wachochole itakuwa ajabu ya kondoo kucheka kioo." Akasema kwa ufasaha.

Maneno haya yalikuwa uzinduzi katika maisha yangu. Ghafla, niligundua kwamba kwa vyovyote vile sikuwa nimefungwa kamba wala kudhibitiwa na uhitaji wa aila yangu. Niligundua kuwa elimu ni ufunguo wa milango yote ya heri maishani. Tangu hapo, nikaamua kuvalia joho la matumaini na jitihada maishani. Dama naye alifedheheka, akaniomba radhi na kumshukuru Tumaini.

Mambo haya yalifanyika miaka kadhaa iliyo kisogoni. Siwezi kughafilika tulivyoungana mimi, Dama na Tumaini kuinamia cha mvunguni katika masomo. Hata baada ya mtihani wa kitaifa, tuliibuka katika nafasi tatu za kwanza kwenye gatuzi letu. Hivi leo, katu sijutii uamuzi nilioufanya kwani nimeyashuhudia matunda yake.

41. Kulingana na aya ya kwanza
A. Tumaini alijulikana maadamu alikuwa mlemavu wa pekee shuleni.
B. ulemavu wa Tumaini ulikuwa mkubwa kuliko wa wanafunzi wengine shuleni.
C. wanafunzi wengi walitumia viti vya magurudumu shuleni.
D. wengi walimjua Tumaini kwa kuwa hawakuzoea kuwaona wanafunzi walemavu.

42. Chagua jawabu lisilo sahihi kulingana na kifungu.
A. Tumaini hakutambua kuwa alikuwa mlemavu.
B. Tumaini alijua namna ya kukabiliana na hali yake.
C. Tumaini aliingiliana vyema na wanafunzi wengine.
D. Tumaini alikuwa mwanafunzi mwenye mahitaji maalum.

43. Shule inaonekana kuwajali walemavu kwa kuwa
A. Tumaini aliweza kuyachangamkia masomo yake
B. wanafunzi wengine walionekana kuhurumia Tumaini
C. miundomsingi iliimarishwa ili kuwafaa wanafunzi hao
D. mwalimu mkuu alijenga choo kipya kitumiwe na Tumaini.

44. **'Maulana alimtunuku Tumaini kichwa chepesi.'** ndiko kusema
A. alikuwa mwepesi wa kuelewa mambo
B. alizoea kujifanyia mambo yake
C. alikuwa mtu wa kulala upesi
D. hakuwa mwepesi wa kukasirika.

45. Walimu walimpenda Tumaini kwa sababu ya
A. hali yake
B. ucheshi wake
C. utulivu wake
D. werevu wake.

46. Taja sifa za msimulizi wa makala haya.
A. Msamehevu, mwenye moyo wa harara.
B. Mtulivu, anayewajali walemavu.
C. Mwenye hasira, anayependa kuchokoza.
D. Maskini, mwenye shingo ngumu.

47. Tumaini alipofika kwenye eneo la mgogoro
A. msimulizi na Dama walikuwa wakipigana
B. alishirikiana na Dama kumdhalilisha msimulizi.
C. alitumia busara kutuliza hali iliyokuwa
D. msimulizi aliona haya akamwachilia mwenzake.

48. Kulingana na ushauri aliotoa Tumaini,
A. kila mwanafunzi ana shida nyingi shuleni
B. vijana wakiyawajibikia masomo wataishi vyema baadaye
C. ni kawaida ya wanafunzi kuvalia mavazi mabovu shuleni
D. mtoto anapaswa kujitafutia mali wala asirithishwe na wazazi.

49. Kifungu hiki kimeonyesha wazi kuwa
A. Tumaini pia ni mwanafunzi kutoka jamii maskini
B. msimulizi alisoma na kuibuka wa kwanza shuleni
C. ugomvi wa Dama na msimulizi utaendelea kwa muda mrefu
D. msimulizi hakuwa na matumaini makubwa hapo awali.

50. Neno **mustakabali** limetumika kwa maana ya
A. maisha ya shuleni
B. maisha ya taabu
C. maisha ya baadaye
D. maisha ya ufanisi.

*TANBIHI: Ili kudurusu kwa kina katika somo la Kiswahili, jipatie nakala ya 'KICHOCHEO CHA KISWAHILI' kutoka Signal Publishers. Kinapatikana katika maduka ya vitabu kote nchini.*